# NOA BONGO JENGA MAISHA YAKO -MASWALA YA JAMII

**Kipindi cha tatu: “Safari ndefu huanza na hatua moja”**

**Mwandishi:Chrispin Mwakideu**

**Mhariri:Maja Dreyer**

**WAHUSIKA: Eveline(19),Mapito(40),Roni(14),Beti(12)
Mjumbe(55),Mwanahabari(27),
kundi(umri wote)**

**1.Msimulizi:**
Karibu tena msikilizaji katika kipindi chetu cha Noa Bongo Jenga Misha Yako kuhusu maswala ya jamii - jinsi ya kuwa mshirika katika siasa. Katika kipindi kilichopita, Roni hakupewa unahodha wa timu yake na Eveline anamweleza babake kuhusu nia ya kutaka kuwa mwanasiasa. Kipindi chetu leo kinakupeleka katika safari. Sio ya kutazama wanyama pori wa bara la Afrika kama watalii, bali kumtizama Eveline akiwa katika safari yake ya kisiasa. Karibu katika safari hii ndefu inayoanzia nyumbani kwa Mapito.

**Onyesho la kwanza: chumba cha kuishi cha familia ya Mapito**

**SFX: KELELE ZA FAGIO ZIKIFAGIA SAKAFU**

**2.MAPITO:** Eve, Eve.. tosha, hawa wanaokuja ni rafiki zako ambao mulikuwa pamoja shuleni… sio wapelelezi wa usafi…

**3.EVELINE**: (**akihema**) Lazima niwaonyeshe mfano mwema.. Wataniamini vipi kwamba ninaweza kuongoza juhudi za kuusafisha mji wetu kama nyumba yetu itakuwa kama zizi la nguruwe?…

**SFX: MLANGO UNABISHWA**

**4.MAPITO** :Oh wageni ndio hawa wamefika…Karibuni! Karibuni! hawatajiki… naenda ndani kujisomea gazeti la leo….

**5.EVELINE**: Karibuni… jamani karibuni.. na kweli mumefuri. Sikutarajia mtakuwa wengi hivi … Oh jamani nimefurahi.. wageni ni baraka… kaeni popote pale mtakapo…

**(SFX: MIGOROGORO KIDOGO WANAPOKETI)**

**6.EVELINE**: Nashukuru kwa kuukubali mwito wangu kupitia ujumbe mfupi na barua pepe nilizotuma… karibuni sana…nafurahi kuwaona..

**7.SAUTI**: Katu hatungelikosa! Nyumba yenu inapendeza sana…. Mmmwwwa!

**8.EVELINE:** Shukrani! Asanteni kwa pongezi… sasa tungelianza ratiba yetu… nafahamu kuwa wengi wetu hapa aidha tulimaliza shule ya sekondari mwaka jana na hatujaajiriwa au tuko chuoni.. kwa hiyo msijali sitawaomba msaada wa fedha kwa ajili ya kampeni yangu.. lakini, nawaomba muda wenu na nguvu zenu katika harakati za kuusafisha mji wetu…tukusanye takataka na tuoshe magari….

**9.SAUTI**: Nilipendezwa na hoja zako nilipoisoma barua yako pepe. Lakini Eve, ama nikuite diwani Eve.. unadhani mpango huu utafaulu?

**10: SFX: NUN'GUNIKO NA UCHESHI KUTOKA KWA WAGENI**

**11.EVELINE:** Hakuna lisilowezekana..Kazi hufanywa na wafanyakazi rafiki yangu.. muhimu ni nia… Na tunafanya hivi kuonyesha mfano kwa vijana wazembe na pia kwa baraza la mji

ambalo limeshindwa kukusanya takataka na kusafisha vyombo vya usafiri wa umma.

**12.SAUTI:** Lo! Eve, kweli wewe ni jasiri…tulifikiri siasa ni ya wazee pekee…

**13:SFX: KICHEKO KUTOKA KWA WAGENI**

**14.EVELINE**: Hiyo ndiyo sababu niliamua kugombea kiti cha udiwani kuwadhihirishia vijana kwamba inaezekana kuwa sehemu ya uongozi wa kisiasa. Uongozi ni wetu vijana…waelezeni majirani wetu kuhusu nia yangu.. hata chifu wetu nimemueleza na amenipa ruhusa ya kuendeleza harakati hizi kutoka kwa mamlaka…

**15.SAUTI:** Basi tuzipotezeni wakati….Tuanze kazi mara moja..tuna jiji la kusafisha.

**16.MSIMULIZI**: Kwa hatua hiyo moja na ndogo, Eveline na marafiki zake wameanza safari ambayo vijana wengi wangeiota tu! Lakini hata hawakujua yale yanayowasubiri mbele yao…Beti naye ana habari kwa kundi lake la uimbaji.

**<u>Onyesho la pili: Beti na wenzake</u>**

**SFX:KENGELE INALIA NA WANAJIFUNZA WIMBO WA "MALAIKA"**

**15.BETTY**:Kumradhini wenzangu.. leo sitaimba nanyi kwani nataka kwenda kumsaidia dadangu ambaye anafanya usafi katika jitihada yake ya kuwa mwanasiasa na hasa, kuwa diwani..

**16.BINTI**: Huwezi kutuacha nyuma, kwani sisi hatuwezi kuja kusaidia? Hata tunaweza kutumbuiza kwa nyimbo zetu wakati wa usafishaji… ama?

**17.BETTY:**Hilo ni wazo zuri! Nina hakika dadangu atakuwa na furaha pomoni kwani anahitaji kila msaada.

**18.BINTI 2**: Mimi simo! Wanasiasa wote ni walaghai na wezi!

**19.BETTY**: Hapana! Wapo walio waadilifu… dadangu ni mmoja wao..na pia yupo Nelson Mandela… dadangu ana mpango wa kufanyia usafi watu wote na hata kwenu tutakutembelea..anapenda watu wote wa eneo hili.

**20.BINTI 2**: Samahani Beti, lakini mimi siko tayari kuongozwa bila kujua niendeko na wewe… hata mimi nina maisha yangu… pole…

**21.BETTY**: Ndio nafahamu… maisha yako ya kujitosa katika mapenzi ya kiholela na kujidanganya… Kundi letu limetuweka pamoja na tunapeana ushauri, tunafanya kazi za shule pamoja ili tufaulu katika masomo yetu na hata uimbaji wetu… hata hivyo, hukukosea… hayo ni maisha yako… wenzangu twendeni.. akibadili mawazo atakuja kukutafuta, anajuwa pakutupata…

**<u>Onyesho la tatu: maosheo ya magari</u>**

## SFX: WASICHANA WAIMBA NYIMBO YA MALAIKA NA SAUTI ZA WATU WAKIFANYA KAZI ZASIKIKA

> **1.MWANAHABARI**: (**akiripotia**) Mpenzi msikilizaji popote ulipo hii ni stesheni yako ikikuletea matangazo moja kwa moja kutoka hapa, tukishuhudia vijana wengi wakiosha magari, wengine wakikusanya takataka na kusafidha barabara… yote haya yameandaliwa na si binti chipukizi Eveline Mapito ambaye tumekutana naye hivi sasa…. Eveline, hebu mueleze msikilizaji juu ya haya yote…

**22.EVELINE**: Kusema kweli jamii yetu imetupa mengi sisi vijana

na nilihisi huu ndio wakati nasi kuipa jamii shukrani zetu… Nimeandaa zoezi hili la usafi na marafiki zangu ili kuwajumulisha vijana wasio na ajira na pia tuusafishe mji wetu. Pia ninafanya hivi kuwadhihirishia watu kwamba ninataka kuwahudumia kama diwani wao..

**23.MWANAHABARI**: Eveline Mapito, wewe una umri wa miaka kumi na tisa tu, maono yako ni makubwa sana… naliona gari la mbunge wetu linakaibia.

**SFX: GARI INASIKIKA IKIFIKA NA KUSIMAMA**

**24.MWANAHABARI**: Tafadhali muheshimiwa, napenda kukuuliza swali moja.. sio lazima utoke garini mwako.. muheshimiwa, unaonaje kuhusu muamko wa Eveline katika siasa, na hasa ambavyo hayuko katika chama chako?

**25.MJUMBE**: Ninafikiri nini? Kwanza, ana haki ya kusimama katika siasa kama katiba inavyomruhusu, lakini nasikitika hawezi kuambulia chochote! Miaka kumi na tisa? Muarifu asipoteze muda wala maji yake, kueneza tope na mbu bure! Hii ni siasa na katika siasa ni mababe tu wanaofaulu…( **kicheko na stihizai**)

**26.MWANAHABARI**: Mheshimiwa, usafishaji aliouandaa umefaulu pakubwa! Sijaona vijana wengi wakiwajibika mahali pamoja bila malipo kama leo…

**27.MJUMBE:**Tafakari…mimi nimekuwa katika siasa miaka mingi kabla ya yule binti kuzaliwa.. na ninakuhakikishia kuwa hatoweza kumshinda diwani wa chama changu…

**28.MWANAHABARI**: Huyo alikuwa mjumbe wetu. Sasa turudi tena studi

**MUZIKI UNASIKIKA**

**29.RONI:** Kumradhi mheshimwa, ni lazima uwe mjumbe wetu… mimi naitwa Roni na hapa tunaendelea na shughuli za uoshaji magari…

**30.MJUMBE:** Wacha porojo kijana! Hebu tazama vizuri… hii si gari ya kushikwa na watu wa tabaka lako…hii gari imenigharimu sana! Nimeitoa Ulaya! Licha ya kuosha, hata kushika usithubutu!! (**AMFOKEA RONI**) Niondokee! Kabla sijakuitia askari. Mjinga wewe! Dereva hebu twende !!!

**SFX: GARI YA MJUMBE YAONDOKWA KWA HARAKA**

**31.MSIMULIZI:** Hivyo ndivyo walivyo viongozi wetu wengi… Wanasahau umuhimu wa wakaazi wa eneo wanaloliwakilisha bungeni…waajiri wao… Mbunge amekataa gari lake lisioshwe, lakini wakaazi wa Milimani wamefurahia msaada. Baada ya zoezi hili wengi wametoa michango yao ya kifedha ingawa Eveline hakuwaomba…Familia ya Mapito inajiandaa kurudi nyumbani…

**<u>Onyesho la nne: mapito na familia yake wanarudi nyumbani baada ya kuosha magari</u>**

**32.MAPITO:** ( **kicheko**) Oh kijana wangu maskini, mbunge amekwambia nini?

**33.RONI**: (**AKIMUIGA MJUMBE**) Hii ni mercedez benzi.. ndani iko na mtandao kutoka Ulaya…ya daraja la kwanza ina SMS au kitu kama hicho.. inatisha! Niliogopa sana hata singeweza kuelewa alichokuwa akisema.. Watu kama hawa wanawezaje kuwa viongozi wetu?

**34.EVELINE**: Mamlaka yamewaharibu.. subiri nitakapokuwa diwani.. watarekebishika! Nataka nilete mabadiliko…

**35.BETTY**: Dada, tumefurahia sana zoezi hili… ni lini tena

utakapoandaa tena?
**36.EVELINE**: Nafahamu hivyo… hata mimi nilipenda uimbaji wenu… wakati mwengine.. tutasafisha hospitali na zahanati zetu…

**37.MAPITO**: Eveline, sitaki ufikiri kuwa wewe unaweza kusuluhisha shida zote za jamii hii.

**38.EVELINE**: Najua siwezi baba, lakini ni vyema niwe miongoni mwa wale wanaosuluhisha badala ya kuwa sehemu ya tatizo..

**39.RONNIE**: Ala. Sasa watu wamekuchangia pesa ngapi?

**40.BETTY**: Ndio ngapi,eh?

**41.EVELINE**: Jumla ya shilingi elfu hamsini..

( **RONNIE NA BETTY WASHANGILIA)**

**42.EVELINE**: Nashukuru kwa kuwepo kwenu…

**43.MAPITO**: Bila shaka tuko pamoja, sasa pesa ziko wapi….

**44.EVELINE**: Tayari nimezipatia kamati tulioibuni katika mkutano leo asubui na kesho zitapelekwa benki…

**45.MAPITO**: Vyema! Kwa sababu wjua pesa ni ibilisi… bora kuzihifadhi na kupanga matumizi yako kabla ya kutumia…

**46.EVELINE**: Baba, napenda kukuuliza kama waweza nisaidia…

**47.MAPITO**: Bila shaka, bora tu usiniambie niende kukusanya mapipa ya takataka…

(**WOTE WANACHEKA)**

**48.EVELINE**:La hasha. Siwezi kukuuliza kufanya kitu kamahicho..Ningependa uwe mshauri wangu hivi kwamba

ninapozungumza na kamati yangu uwe unaweza kunipa maoni yako..

**49.MAPITO**: Maoni yangu kama babako au kama mshauri wa kampeni yako?

**50.EVELINE**: Hmmmm, labda tusema yote mawili..

**51.RONNIE**: Afadhali tumefika nyumbani.. nimechoka sana .. naenda kulala moja kwa moja… tuonane kesho. Usiku mwema wanangu..

**SFX: FUNGUO ZASIKIKA ZIKIFUNGUA MLANGO**

**52. MAPITO**: Eeeh…Roni… kesho kabla ya kwenda shule.. nataka kuzungumza na wewe…

**MWISHO WA KIPINDI CHA TATU**

**Msimulizi:**

Akiwa mchovu lakini mwenye furaha kwa kufaulu kukabiliana na changamoto yake ya kwanza, Eveline alikwenda kujipumzisha kitandani. Jiunge nasi wiki ijayo huku hadithi ya familia ya Mapito ikiendelea kufichuka. Utasikia vipi mbunge atakavyoupokea mpango kabababe wa Eveline na ujifunze vipi Roni anavyohisi uchungu wa kushindwa huku Beti akifaulu tena. Kisikilize tena kipindi hiki katika tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe. Hadi wiki ijayo kwaheri!